

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAISI-TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA BARIADI
SHULE YA SEKONDARI IKINABUSHU**

S.L.P 255,

BARIADI.

Barua Pepe: *mdongomashaka78@gmail.com*

TAREHE _____

KUMB. IKSS/BDC/J.1//VOL.16

NDG. MZAZI/MLEZI WA _____

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI
IKINABUSHU KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari **IKINABUSHU** mwaka wa masomo 2021. Shule hii ni ya kutwa na mchanganyiko (Wasichana na Wavulana). Hongera sana.

Muhula wa masomo utanza tarehe **11/01/2021**. Hivyo, mwanao anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021** kwa ajili ya usajili na kuanza masomo. **MWISHO WA KURIPOTI NI TAREHE 22/01/2021, ENDAPO MWANAO HATAFIKA AU KUCHELEWA KUFIKA HATUA KALI ZA KISHERIA ZITACHUKULIWA DHIDI YAKO WEWE MZAZI/MLEZI**. Ni jukumu la mzazi/mlezi kuhakikisha kuwa mwanafunzi anawahi shuleni bila kukosa au kuchelewa baada ya kukamilisha mahitaji na taratibu zote zilizoелеkezwa katika barua hii.

MAHALI SHULE ILIPO:

Shule ipo wilaya ya Bariadi Vijijini, tarafa ya Dutwa kata ya Gilya katika Kijiji cha Ikinabushu. Umbali kutoka Makao Makuu ya Wilaya ya Bariadi ni Km.46, na umbali kutoka Makao Makuu ya Halmashauri ya Bariadi Vijijini ni km.10 (kutoka Dutwa).

MASOMO YANAYOFUNDISHWA SHULENI:

Atakapo kuwa hapa shuleni atapaswa kusoma masomo tisa 9 ambayo ni **CIVICS, HISTORY, GEOGRAPHY, ENGLISH LANGUAGE, KISWAHILI, PHYSICS, CHEMISTRY, BIOLOGY, BASIC MATHEMATICS**. Masomo yote yanafundishwa kwa lugha ya kingereza isipokuwa somo la kiswahili. Lugha ya mawasiliano shuleni ni kingereza tu.

MAHITAJI:

A. NDANI YA DARASA

1. Daftari kubwa za kutosha
2. Mathematical set 1
3. Kalamu za wino na penseli za kutosha
4. Mfuko wa madaftari (school bag)
5. Kamusi ya kingereza – kingereza {dictionary}

B. SARE YA SHULE:

1. **WAVULANA:** Awe na shati mbili nyeupe mikono mifupi, tai mbili Nyeusi na viatu vyeusi vya ngozi vyenye kufungwa kwa kamba, soksi nyeusi jozi mbili, suruali mbili rangi ya Nyeusi (suruali iwe pana siyo chupa (Model) chini yenye turn up, iwe na mifuko mitatu miwili mbele na mmoja nyuma) na sweta rangi ya kijani.
2. **WASICHANA:** Awe na blauzi mbili mikono mifupi na tai rangi nyeusi, viatu vyeusi vya ngozi visigino vifupi, soksi nyeupe jozi mbili, sketi mbili rangi ya nyeusi, kitambaa kizito, sketi iwe **NDEFU** kuvuka magoti kwenda chini, sweta rangi ya kijani.
3. **SARE YA MICHEZO:** Track suti bluu kwa wavulana. Kwa wasichana Track suti blue, raba za michezo jozi moja 1.

NB: MAVAZI YASIYO YA HESHIMA HAYATAKIWI

Sare ya shule itavaliwa wakati wote mwanafunzi awapo shuleni, darasani, shughuli zote za kishule na wakati wa safari nje ya shule. Katika michezo kila mwanafunzi atatakiwa kuvaa sare ya michezo iliyoelekezwa katika fomu hii.

4. **VIFAA VYA USAFI:** Mwanafunzi anatakiwa kuja na ufagio wa nje (chelewa), ndoo ndogo ya lita 10 na jembe moja kwa ajili ya shughuli za usafi na kazi za mikono(shamba la shule).

ANGALIZO

- Ni marufuku kwa mwanafunzi kuvaa viatu vya ghorofa (visigino virefu)
- Ni marufuku kwa mwanafunzi kuvaa nguo zisizo rasmi shuleni
- Ni marufuku mwanafunzi kuvaa suruali mlegezo(kata K) na ukibainika hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yako
- Kila mwanafunzi anapaswa kuwa safi, kufanya usafi kikamilifu katika eneola shule alilopangiwa kila siku
- Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu kanuni, taratibu na sheria za shule. Hivyo, lazima awe na nidhamu ya hhali ya juu.

C. MIPAKA YA SHULE

Kila mwanafunzi atatambulishwa mipaka ya shule na kuifahamu. Hivyo,

- (i) Ni marufuku mwanafunzi kuwa nje ya eneo la shule katika muda anaotakiwa kuwepo shuleni bila ruhusa maalumu.
- (ii) Ni marufuku kutembelea sehemu zifuatazo hata kama sioi muda wa shule:-
 - Nyumba za kulala wageni(Guest house/Lodge)
 - Vilabu vya pombe(Bar)
 - Nyumba za walimu na Ofisi bila kibali
 - Kumbi za starehe

Pamoja na barua hii, nakufungashia fomu mbalimbali ambazo ni lazima zijazwe kikamilifu kabla ya kusajiliwa na msajili wa wanafunzi ha shuleni. Fomu hizo ni pamoja na sheria za shule, taarifa binafsi za mwanafunzi na vipimo vya daktari

(Medical Examination Form) na uthibitisho wa mzazi/mlezi.

KARIBU SANA IKINABUSHU SEKONDARI

**MASHAKA MDONGO
MKUU WA SHULE
0689 481 720**